
# ASIFIWE BWANA MUNGU

"Wimbo wa Zakaria"

Aron Reginald




>Aliahidi hapo kale ,* Kwa njia ya manabii wake watakatifu.

>Kwamba atatuokoa kutoka maadui wetu ,* Na kutoka mikono ya wote wanaotuchukia.

>Alisema kwamba atawaonea huruma wazee wetu,*na kukumbuka agano lake takatifu.

>Kwa kiapo alichomwapia mzee wetu Abrahamu/aliahidi kutukomboa kutoka maadui wetu,* na kutujalia tumtumikie bila hofu.

>Ili tuwe watakatifu na waadilifu mbele yake,*siku zote za maisha yetu.

>Nawe mwanangu utaitwa,*nabii wa Mungu aliye juu.

>Utamtangulia Bwana,*kumtayarishia njia yake.

>Kuwatangazia watu kwamba wataokolewa,*kwa kuondolewa dhambi zao.

>Mungu wetu ni mpole na mwenye huruma/atasababisha pambazuko angavu la ukombozi,* litujie kutoka juu.

>Na kuwaangazia wote wanaokaa/katika giza kuu la kifo,*aongoze hatua zetu katika njia ya amani.

>Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu,*kamamwanzo na sasa na siku zote/na milele. Amina.